



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))



Kumb.Na. L.10/7/AB/25

08/03/2024

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga anawatangazia Watanzania wenyе sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kuomba nafasi za kazi zilizotajwa hapo chini, baada ya kupokea kibali chenye **Kumb. Na. FA.228/613/01/010** cha tarehe **22 Disemba, 2023** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

1 DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 2

1.0 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV).
- Leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundı Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Waombaji wenyе cheti cha Majaribio ya Ufundı Daraja la II watafikiriwa kwanza.

1.1 MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- (ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- (iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- (iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- (v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- (vi) Kufanya usafi wa gari na

(vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyo elekezwa na Msimamizi wake.

1.2 NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya mshahara ni TGS B.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenyewe umri usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini serikalini;
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili;
- iii. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayo jitoshleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya **Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Cheti cha Kompyuta, Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)** “Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) HAVITAKUBALIWA.
- vi. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**
- vii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka **Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **22 Machi, 2024.**

- x. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA,
S.L.P.716
MWANGA

- xi. *Maombi yote zitumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu ilioandikwa ‘Recruitment Portal’).*
- xii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**
- xiii. Limetolewa na;

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA
MWANGA

Barua zote zitumwe kupitia anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, , S. L. P 716, **MWANGA**, Simu +255 26 2757652, Nukushi + 255 26 2756463, Baruapepe; ded@mwangadc.go.tz, Tovuti www.mwangadc.go.tz